Mzee Musa Jaka: Jina langu naitwa Mzee Musa Jaka, na mimi ni mwana harakati wa trade union. Na hapa niko na maswali manne. Swali langu la kwanza liko chapter 5 katika Bill of Rights ambapo tumeambiwa kuna political rights ambapo utakuta kwa sasa mfanyi kazi yeyote ya Serikali ama wa parastatal board yeyote haruhusiwi kusimamia ubunge mpaka wakati ataacha kazi ama kufanyia campaign chama fulani ama vyote. Hapo tunaambiwa anayo political rights ndiyo lakini sasa hatukwaambiwa je anao uwezo wa kusimama kabla hajaacha kazi ambapo ikiwa atapata kile kiti aendelee aache kazi lakini hakupata arudi kazini. Katika hii Constitution mpya hatukuambiwa wakati kule nyuma tuliambiwa kwamba mpaka aache kazi ndio aweze kusimamia kiti lakini tulipendelea mtu hata kama uko kazini asimamie kiti cha ubunge au councilor akipata then aache kazi.

Halafu swali langu la pili katika hiyo hiyo Bill of Rights, kuna rights to a worker to have fairly remuneration. Sasa utakuta kwamba kuna wanafanyi kazi tunaita kibarua. Mfano kibarua anaweza kufanya kazi katika idara fulani ama kampuni fulani ile design ya mhindi ama mtu yeyote. Lakini mfanyi kazi yule katika sheria tunaambiwa kwamba ana miezi sita ya kufanya kama kibarua lakini utakuta anafanya miezi mitatu anasimamizwa, halafu anarudishwa baada ya miezi mitatu, anafanya miezi mitatu anasimamizwa sasa pale unakuta hakuna fairly remuneration na hapa tunaambiwa kuna fairly remuneration lakini hatukuelezwa je itakuwa vipi kwa mfanyi kazi wa kibarua kama ile. Sisi tungependelea kama ni fair remuneration, yule mfanyi kazi akiajiliwa

ajiliwe straight away bila kuwa kibarua kwa sababu tunaona wengi sana wanatesheka.

Halafu tuna the Right to Strike: Unakuta chama kinatoa notice ya ku-strike labda ile 21 days inakwisa wana-strike lakini hapo hapo tunaambiwa kwamba ile strike ni illegal. Wafanyi kazi baadaye wanafutwa. Sasa pale the right to strike hakuna. Sasa sijui hii Katiba mpya hiyo right to strike iko kwa njia gani hatukuelezewa pia.

Halafu swali langu nne liko katika chapter 11. Mambo ya lands hapa tuna absentee landlords wengi sana. Utakuta mtu ana kisauni nzima ile shamba ni lake. Lakini nyumba ni za watu wengine wa club ambapo yeye mwenyewe haizi pale. Sasa katika hii Constitution mpya hatukwambiwa absentee landlords, Serikali ina nia gani kusaidia watu kama wale ambao wamejenga sehemu ya Kisauni wa na nyumba zao pale lakini landlords mwenye ile ardhi lets say yuko ngambo ama yuhaihi huko nguze ya masimu wale ambao tunaitwa mabwanyenye ambao wanatawala zile ardhi. Hatujaelezewa katika hii Constitution mpya Serikali ina nia gani ama itasaidia sisi wapi.

La mwisho; Sheria tulikuwa na Constitution ya nyuma ambapo ilipitizwa wakati wa uhuru, lakini kuna sheria nyingine ambacho zinatufaa sisi wananchi. Ni nzuri ziko zinaendelea lakini zilikuwa hazikuozi na ni kwa sababu ya ubinafsi wa watu. Na hii pia ni Constitution vile vile, haya ni maandishi hatujui atakayaingia atakua vipi. Je ni njia gani ambao itafutwa kuhakikizwa kwamba Constitution hii inafuatwa kulingana na sheria. Yaani mtu asichukue mamlaka kama vile Rais sasa ama mawaziri. Utakuta waziri anashitakiwa lakini yule msitaki akienda kule kortni ndiye anapata haki. Sheria ni hizi zinandikwa lakini hazifuati, je tuna hakika gani kwamba sheria hii zinafuatwa? Asanteni.

Com. Salim: Namba ya saba?

Abdul Rahmani Ali: Salaam aleikum. Habari zenu wengine ambao sio Waislaam? Jina langu kamili naitwa Abdul Rahmani Ali. Natoka katika kikundi cha harakati ambaye kinafamaaka kama Zingaro Environment Youth Group. Nimekuja kidogo nina maoni mawili, matatu. Kwanza nawashukuru kwa kazi yenu nzuri mliofanya Bwana Professor na wezako wote, halafu vile vile nasukuru kwa hii Katiba ambayo tumepitia pitia kidogo tumeona mambo ambao iko ndani si ma mbaya sana. Lakini kulikua kuna kitu kizizitisha kama mwezangu aliondoka hapa amesema ile kuzizitiza kwamba Katiba hii itakuwa na uhakika gani kwamba itafuatwa kama vile alivyosema kwamba siku ya ukoloni pia haikua mbaya bwana zingine ni nzuri, lakini vile hakikisho kwamba kweli itatimika na wakipewa wale wateleka. Njia gani ambayo hata wakitunyima ile haki yetu sisi wananchi tuwe tunaweza kuwa tutakuwa na jukumu wa kuweza kusukuma wasipitimizwa, hiyo ni moja.

Pili nilikua nazungumzia zaidi kuhusu mahakama, maana yake nimeona mahakama zetu hapa zimepewa uwezo wa hali ya juu sana ambalo ni kosa kubwa. Sasa, nimeona kwamba Katiba hii inasema kwamba zingine ikiwa itakubalika hawa judge wengine lazidi wa-sign upya ama sio vile nilivyolea. Hata kwa hiyo tulikua tunaomba kama itakuwa wana-sign upya at least ikijaribu kufuata kama mifano wa nchi zetu jirani imetembea kidogo tukaona kwa mfano kama hapa Tanzania ilikuenda kidogo.

Nikatembelea sehemu za mahakama zao nikaona zinapata haki ya kisawasawa. Shauri zile mahakama zenyewe zinaanzia gazi ya chini masinani. Utakuta kule mahakamani labda kuna balozi wa nyumba kumi, halafu kuna wazee wa mitaa ambao wanakaa kado ili kujadiliana na yule hakimu. Kuihukumu kesi ya yule mshtakiwa. Sasa iwapo yule mstakiwa labda pengine amedhulumiwa maana hapa kwetu Kenya tunaona wengi wafungwa pale ni suspect. Wale waliofanya makosa makubwa makubwa wote tunaona wako nje mpaka leo. Lakini ukitembelea magereza kwa mfano kama mimi niko katika human rights groups tulitembelea Shimo La Tewa tukahoji watu maswali pale. Tukakuta katibu aslimia kumi na tano yote wamefungwa bila makosa ni vile hawa watu wa kusimamia na hajui sheria na wala hakuna pale kortini pakazimika tu ujanja akificha yule maskini, lakini yule ambaye anahusika kupelekwa pale akatolewa kwa ajili ya uwezo fulani.

Hata kwa hiyo kama tungekuwa tunaona hapa kwetu Kenya sio kulingana na hii Katiba mpya vijeongezewa kwamba haya mambo ya sheria ingaazia huko gastani ili tuwe kuweza na wazee wa kadhaa na akina wama kadhaa kama wawili watatu kama tunaambiwa na jirani wetu Uganda, Tanzania, wanaweka wale wazee, mzee anaweza kujuwa huyu bwana huu kijana ni mwizi mimi namjua kabisa, sasa iwapo atamzongea Judge bwana ni kweli kazi yake. Nyingine yaweza ikapatikana haki.

Halafu swala la mwisho kabisa ni hizi swala la ardhi. Mimi nashangaa sana kuona hapa kwetu kwamba kuna Ministry of Lands.

Wakati hiyo ministry yenyewe haina land yeyote, land zote zimemilikiwa na watu binafsi. Lakini nashangaa ile ministry kazi yake nini imewekwa pale. Na afadhali kama haingekuwa kabisa. Shauri hizi land za Kenya hapa kwetu tuna squatters in zaidi ya ma million ya squatter katika nchi ya Africa zima sisi tunaongeza kwa scattered Kenya. Tukiangalia ndugu zetu Nairobi wanalala kwenye slams, tafadhali Mombasa kidogo, na miji miinginevyo. Hasa tulikua tunaomba kama inawezekana sijui iliyo fungu kwamba hizi ardhi zote zitemeshwe bahati yake kwanza. Iwe ni kama sababu ya kuweza kuzuia ile grabbing.

Unajua sasa hivi watu wengi wana grab ardhi kulingana na ardhi yenyewe ya Kenya yamewekwa zamani ya chini sana. Kiwango mtu akiwa ni ardhi kidogo cha bicha anachukua sasa milioni hamsini. Unaona hata kama ingekuwa hii faini lingetelemshwa kidogo chini nafikiri hazingekuwa kuna mtu anataka kunyakua, utanyakua kitu cha sumu uweke? Unanyakua kitu cha sumu uwezi? Kwa hivyo napigania kunyakua kwa kwamba kina value yake imewekwa juu na ndiyo kwa hivyo kwa sababu mahalai unawadwa ni huko juu. Kwa hivyo ndio langu la mwisho la ardhi.

Benson Masika: Asante Professor na Coordinators vile mmejitolea kuja kuchukua yale mapendekezo yetu ambayo yalikuwa yametolewa. Kwa jina yangu naitwa Benson Masika kutoka kanisa la Seventh Day Adventist Church. Katika mapendekezo ambayo nimeyaona, kuna machache ambayo nataka kutoa maoni juu yake ili mweze kuangalia. Ni juu ya Education. kuhusu elimu nimeona ya kwamba mmependekeza ya kuwa private institutions ama watu wanakua na private institutions ama watu wamaliwa ma private institutions these universities and colleges baada ya kupewa chati na kujulikana ya kwamba zinafuzu vizuri wanafunzi wao wakimaliza baada ya graduation hawapati kazi, ama wakati mwingine wanachwa nje. Hilo jambo liweze kuangaliwa kwa sababu ikiwa mitihani na masomo yale ambayo wanahitimu ni kama yale ambayo yako public universities ni vizuri waweze kuwangaliwa.

Na jambo lingine kuhusu hicho private institutions wakati mwingine zinatoshia bei ya juu kwa sababu gani. Sababu hawapati msaada wowote kutoka kwa Serikali. Serikali ingeangalia kwamba wanapokuwa wanasaidia katika latola njia hiyo kuandeleza elimu ama kwa matibabu, ni vizuri pesa zitengwe pia kama grants za kuwasaidia ili maana watoto wale ambao wanasoma pale ni watoto wetu, ni watoto wa Kenya waweze kuangaliwa pia ili hata ile gharama iweze kurudi chini. Kwa sababu ile fees ambayo wanatoa ni kwa sababu hawapati msaada kuto mahali popote nina kumbuka zamani tulikuwa tunapata misaada kutoka ngambo ambayo ilikuwa ilikuja kusaidia hapa Kenya. Lakini siku hizi hakuna nchi yeyote ambayo inaweza kuleta msaada wake hapa Kenya. Ni Kenya tu peke yake ambaye inaweze kujiendeleza na kwa hivyo sisi kama wana-Kenya na tunaona jambo ile ni nzuri tuweze kulifanya ni vizuri Serikali iweze kutia mkono wa kusaidia.

Swali la mwisho ama pendekezo la mwisho ni kuhusu matibabu, health. Kuhusu Health nimeona ya kwamba watu wanaweza kupewa matibabu, lakini sasa kuna hii kitu kinaitwa cost-sharing. Na mahali pengine unaweza kupata kwamba, huyu ambaye amekua .mgonjwa hana njia yeyote ya kuweza kutoa fedha ila apate yale matibabu. Ni vizuri Serikali iweze kuangalia kwamba jambo hili la cost-sharing, uhai wa mtu uweze kuangaliwa vizuri ili matibabu yaweze kuwa ya bure. Kwa sababu kuna system ambacho zimewekwa ya kuhakikishwa ya kwamba mwananchi anapotozwa kodi, ile kodi iliyo kazi yake ili iweze kuangaliwa vizuri maana nafikiria kwamba hii cost-sharing ilikuja kwa sababu there was misappropriation of these funds katika Serikali. Kwa hivyo wakaona sasa wabuni njia ingine ili wananchi waweze kutoshwa wapoenda kwa matibabu. Na kwa sababu Constitution hii yetu ambayo tumependekeza iweze kuangalia vizuri ili pesa zote ambazo zinatozwa kutoka kwa kila jambo liweze kuangaliwa vizuri na misappropriation yake ifanywe vizuri. Ni hayo tu ambaye naweza kusema na asanteni.

Michael Kiti Nyanje: Mimi naitwa Michael Kiti Nyanje. Nilikuwa nina mambo fulani ambayo nilikua nitaka kuzungumzia. La kwanza ni kuhusu elimu. Tumeona katika ile mapendekezo yenu mmesema kutakua na elimu ya bure ya primary, lakini nafikiria hamkusema hii ya nursery pale ndani, ikiwa pengine umesema pengine mimi sikuiona. Kwa hivyo mapendekezo yangu ningomba kua hata hii ya nursery pia hivyo itakua ya bure. Yaani Serikali iandike walimu wa kufundisha nursery.

Pia kuhusiana na elimu tunaomba, ama ninaomba ama natoa pendekezo ya kuwa kila province iwe na university moja. Tena na hapa pwani ambao tunaona kuna Waislaam wengi pia Serikali ione kuwa tunapa university moja ya Kiislaam.

La pili ni kulingana na uchaguzi. Nimesoma pale nikaona kuwa mapendekezo ya kwamba a third of candidate from an individual party to be women. Lakini naona mimi kuwa pengine itakuwa kwa sababu hawa watu wanachaguliwa na watu wenyewe, raia wenyewe. Naona kuwa pengine itakuwa uwe shida kwa chama. Pengine wale nominated it is okay, but these one who are elected directly I think it is not going to be applicable.

Lingine, ni kuhusu qualifications za National Assembly that power Nikisoma pale nimeona mmeandika mtu awe amefikie kidato cha nne na awe amepita mtihani lakini hamkusema ni kiasi gani hapo, mtu anaweza na D- na atasema tu amepita mtihani.

Mimi nilikua nimepita mthani. Kwa hivyo nimeonelea angekua na kama ningesema it is a degree and above or C and above. Na pia kwenye hizi councils qualifications zake pia ziwe kama D+ ama degree ya kitambo.

Jambo lingine ni kuhusiana na refugees. Tunajua sheria za refugees za kimataifa lakini unaona hapa kwetu Kenya, sisi sheria hizo hatufuati tunaona refugees wamehusiana na sisi, wananchi na sisi, unaona hata kuna wengine kabisa wamepata kitambulizo wanafanya biashara kama Wakenya ambao mimi ningependekeza hiyo Constitution mpya, ikiwa inafanya kazi hawa refugees ambao wamepewa kitambulizo ya Kenya wapokonywe na wawekwe mahali pamoja kama safety place ambapo wanafaa wawekwe.

Jambo lingine ni kuhusu ministers. Ministers napendekeza ni kumi na watano hiyo ni sawa, sasa ningependa kuongezea pale hawa ministers ningependekeza kua wawili watokezee kwa kila province, tena they should be indigeneous people hata mimi by indigenious people those tries which originated from that place.

Then lingine ni kuhusu miji. Ningependekeza miji ambaye imestawi na imendelea kama vile Nairobi tayari imejimudu kuongezea na hiyo Mombasa, Kisumu na miji mingine ambao imestarab kama hiyo ifanywe city.

Com. Salim: City ni wapi?

Michael Kiti Nyanje: Officially haijafanya tu district. Imesemwa tu kisiasa lakini haijafanywa.

Halafu la mwisho kabisa ni kuhusu wajiri i.e recruitment and employment of any kind should comprise at least 75% of the indigenious people of that particular province or district.

Com. Salim: Asanteni sana kwa maoni yetu kwa hakika nilisema hapo awali kwamba hatuna nafasi tunafunga saa sita unusu, maana leo ni ijumaa na swala, wengine tunaelekea kutawaza na kadhalika lakini huenda ikawa maswala na jawabu ya maswala haya ni kutosha hamazisha mtu kusoma zaidi. Lakini tayari kabisa kupata memorandum. Ikiwa hukupata nafasi kuliza swala lako na unapendekeza tafadhali haraka uinandike na tuko tayari kuipokea na kuisoma baadaye na itapelekwa kwa njia fulani katika matayarisho yetu ya National Conference. Lakini kwa leo samahani hawa kumi ndio ambao tutaweza kuwajibu kama tuwezavyo maswala yao.

Kwanza Mzee Mudadi, umeuliza preamble ungependa iwe na values zitajwe, value kwa hakika tumezifiya mbali, goals , principles and values, lakini swala lako kwa nini freedom fighters hawakutajwa ni swala nzuri tumezingatia sana mambo ya freedom fighters na kulikuwa na mswada or draft ya preamble nyingi sana. Nyingine zilikuwemo ni sala fulani kuhusu freedom fighters lakini mwishowe tumaona kwamba tutaja yale tuliotaja maana kuna nafasi kutaja kila jambo lakini huyu msitajabu kwamba tukienda kwenye conference, freedom fighters wengi wata pendekeza kwamba watajwe au at least kwamba ile

msitasali yetu au kupigana kwetu kwa ajili utawala wetu wenyewe au uhuru utakagika. Lakini tunataka kuhakikishia kwamba pendekezo hilo lilikuwa ni kati ya mapendekezo mengi ambayo tulifikilia sana kisa kwamba experience yetu should also be there, kuna pia mapendekezo mengi kwamba tuhitaji kidogo jinzi ambavyo tulitawaliwa na wageni na mwishowe tukapata uhuru wetu, our historic experience na Constitutional experience. Lakini preamble huwa ni fupi sana na there are so many things to put there. Kwa hivyo lazima vitu fulani kwa sasa viwachwe lakini kama nise mavyo hili ni jambo ambalo huenda likabadilika. Na mwishowe tukapata preamble ambao ni tofauti na hii tulionayo sasa.

The Laws of Kenya By-laws sisi tulitaja jina laws at the national level. Tumewacha zile by-laws ambazo zinahusu Local Government. Lakini kwa kuwa tutakuwa na District Government na mambo kama haya huenda pia mabadiliko yakatokea hapo.

Boundaries of Kenya kwa hakika ni kweli kumetokea kutofahamiana juu ya district na cases to be put forward about the..... so we will bear ni mind your proposals and saa zile transcription ikifanywa they would be picked up na huenda ikahitajika kwenye conference.

Defence of the Constitution, hatukusema hasa we have to defend the Constitution but we did refer to .. tumezungumzia, au dokezea mambo kuhusu kwamba Constitution hii ni ya watu na kwa hivyo Constitution hii izipandilishwe kwa urahizi na baada ya kuzungumshia mambo ya defence na kila kitu tulitaja katika ukurasa 39 kwamba subject to provisions of the Constitution Parliament may in exercising Constitutional powers amend by ways of judgment, variation or repeal any provision with the procedure laid down at this article. Lakini tukasema ya kwamba lazima both houses si kutokua na two houses must ganner or get two-thirds majority kabla Constitutional kubadilishwa na hii si jambo la lahizi tena si two-third ya wale watayohudhuria vikao za National Assembly or National Council ambao watapiga kura lazima two-thirds of all the members. Kwa hivyo njia hii nafikiri itaidwa na kuna mambo fulani hapa ambayo tunasema ambayo tunasema hayawezi kubadilishwa bila referendum bila watu kupiga kura wenyewe kubadiliza mashala ile territory ya Kenya, mipaka yetu, bill of rights ikibadilishwa kabisa kama ilivyo mpaka two-thirds of each house wakubali kubadilika. Restructures values and principles of devolution pia ibadilizwe, citizenship na mambo kama hayo.

David Machoka umeuliza habari ya security judges ungependelea kwa mfano kwamba, uliuliza ikiwa security of judges itakuwako lakini ile age of retirement ni 65. Sijui age of retirement for other people hatukuzungumzia hilo maana ulisoma hapo section (inaudible) section tu mahakimu. Kwa hivyo hatuingilia mambo ya civil servants na permanent secretaries kwa hivi sasa ni nafikiri ni 55 kwa hivyo tumeona kwamba imbakie vile vile – 55. Devolution of powers elders will be paid. Yes they will be paid.

Freedom of religion page 8 why not to make sure that there is no comparison to any act why is the word “may” hiyo ni fikira nzuri, lakini na kuhakikishia kwamba mambo haya kuhusu haki ya mtu asilazimishwe kwa mfano jumamosi kwenda shuleni au kuhudhuria jambo lolote kuhusu shule au sport na kadhalika tumezungumshia na jamaa wengi na such kuna two commissioners

who are seventh day 'S.D.A.' Pastor Ayonga na Dr. Maranga .. lakini neno "may" nakubaliana kwamba huenda ikawa haifanyiki au ifanyiike. The right words may be should have been (inaudible) lakini ni jambo ambalo pia huenda kwa conference likaleta majadialiano makubwa na marefu hasa tukiweco people of different religions bila shaka watakuwako pale ni jambo ambalo wewe pia yaweza kuwadikia barua jamaa ambao watawakilisha kwenye conference walileta jambo comment. Mambo haya sio mambo ambao yamemalizika na ni final lakini ni mumetaja jambo muhimu sana.

Mengi, different from shall, kuingine ambapo mmesema kwamba ni lazima ifanyiike tumetumia neno la shall, no one shall be compelled.

Bwana Daniel Okondo, twakushuru sana kwa maoni yako lakini nakuhakishia ya kwamba disabled tumewataja kwa wingi kila hujapata nafasi kuisoma section kuhusu disabled umpewa nafikiri kuna nakala ya Braille utaisoma uzuri tumetaja kwamba ufikirie – umetaja kuwa mishara yao izingatie kwamba wao wana haja ya wasaidizi. Sio? And you feel that their salaries should higher ile yaweza kupata sijui kwamba ni kufaham hapo. Ulikusudia jambo hilo sio? Kwamba mishahara yao izingatiwe kwamba wao watahitajia mtu kuwasaidia kwa hivyo they should be allowed to any one whom they might need to help them their day today activities. Pia ni jambo ambalo tumelinasa na bila shaka zitalingatiwa. Zile passport za disabled to suit their abilities and reliabilities pia ni fikira nzuri ni maoni mazuri na inahusu syllabus za shule.

Bwana Daniel Mwatata appointment of Prime Minister and DPM umesema kwamba umeandika mapendekezo yako juu ya mambo na karibu Bwana ha karibu tutasoma mapendekezo yako juu ya mambo haya uliyoataja nafikiri 1,2,3,4,5,6 tutasoma kwa maakini si kuyataja hapa lakini tutasoma baadaye.

Universities not mentioned in the Constitution, kweli lakini ujuavyo kujenga university katika kila District. Kujenga university ni gharama kubwa sana na ni taabu kwa District kujisimamia kwa upande ya elimu ya juu. Tunavyo sisi ni kwamba University au Chuo Kikuu huwa ni National Government responsibility. Kwa hivyo labda, pendekezo lako tutaliunganisha na pendekezo na mwezetu wa mwisho Michael, ilikua ni Michael alisema kwamba kuwe na University Coast Province, kwa hivyo nafikiri ni pendekezo kwamba ila tukijenga universities tufikilie kujenga na kwa ajili gani ili kwamba universities zizijengwe katika eneo moja ama mawili tu, kuwe na a good devolution if you like of higher education. it is a matter that also will be taken by the way within many other tumependekeza idadi ya tume ambazo zitashugulikia mambo tofauti tofauti kwa mfano tumependekeza councils, – Economic and Social Councils ni council ambao itafikilia umuhimu wa kuhakishwa kwamba tunasaidia uchumi na tunasadia uadhilifu wa kijamii kuwe kila pahali. Kwa hivyo, this is the Social Economic and Education bila shaka councils ambao tumependekeza itafikilia wapi kujenga shule.

Na kadhalika kuna tume ambayo yazingitia mambo kuhusu haki ya binadamu. Kwa hivyo proposals about the building of universities where to build universities can be captured by many many agencies and organizations within the boundaries we are proposing na bila shaka fikira hii ya kuwe na universities, education ambayo ni ya uadhilifu also if you look at the bill, goals and

values and principles, tunasema kuwe na equity uadhilifu kila mahali. So, the issue of university education will be I am sure taken care of within the context of those values and principles.

Employment quotas, nafikiri ulipendekeza kuwa, kuwe employment quotas. Tunasema hapa course wafanyi kazi wa idadi fulani, wa percentage fulani wawe local. Nafikiri ni prayer yako.. Bwana Daniel, ulikuwa ulipendekeza hilo. Sio? Kwamba upande wa employment ulitaja kwamba sehemu fulani ya kazi ipewe wenyeji wa pale or something to that effect probability?

Anyway the main thing is, unajua employment na how to employ itabusana kupitia kwenye Constitution. It is a matter of details, hapa na pale tutasema kwamba, mambo haya hazingaziwe na sheria ya Parliament. Kwa hivyo mambo ya employment, mambo ya kuhakisha kuwa kuwe na uadhilifu katika kazi na jinsi ya kuu... ni mambo ambao yatafikiliwa na sheria nyingine ndogo. Hii ni sheria ya mzee, sheria ya mama kuna sheria toto, or sheria ya watoto, bila shaka mambo haya .. wajua early employment ni matatizo. Kila sehemu ulimwengu ina matatizo ya early unemployment. Na kuna nchi moja duniani ambao haina problem ya employment sema pengine problem yao ni ndogo kuliko wenzao. Lakini you can't possess issue of employment, you can only put Equity uadhilifu na mambo kama hayo. Principles ambazo zaweza (inaudible).

Mzee Musa Jaka – Bill of rights political rights and civil and the politics, tumesema kwamba hili pia ni mambo ambalo hatukutaja in details. Hatukutaja nakubali kwamba mtu asilizamishwe ku-resign kabla hajaweza kusimama kwenye election. Pia, ni fikira ambayo tume inaza na huenda tulizingatie tena watu (inaudible). Tumepata malamiko mengi kwa wananchi kwamba kwa nini civil servants wa-resign kwanza kabla hawaja... kwa nini hawapewi leave of absence? Leave bila kulipwa kwa ajili ya kupoteza kazi zao. It is a matter that.. bila shaka ukisoma ripoti yetu utaona ya kwamba tumetaja hapa na pale.

Fair remuneration of workers when– hatukweza kusema zaidi ya hivyo maana tukisema the rights or the fair salary of a messenger should be so much. The fair salary of a clerk should so much. The fair revenue or remuneration of a doctor in government hospitals should that. Hatuwezi kutaja figures. Fair, maana yake ni adhififu ambayo yamwezesha kuishi bila kupata idhilali bila kupata taabu. Pia, tumezungumshia bill of rights kwa Serikali ina haki ya kumpa kila mwananchi haki zake za kimsingi. Ikiwa maana yake makao, matibabu, elimu na kadhalika imetajika parable moja na kwingine tumetaja fair salaries – sasa sheria ndogo zile au sheria ya watoto kufikiria mambo kama hayo. Industrial courts ndiyo ambayo yakata shauri.

Wajua hii ni Katiba ya kuja – twasemaye kwamba itahishi milele au itaishi miaka mia moja mia mbili, mia tatu kama hii ya America. Kwa hivyo tukiwa na 100 years from now au miaka mia mbili kutoka sasa mambo yatabadilika kabisa. Fair remuneration ya leo si fair remuneration za miaka kumi kutoka sasa. So we can't give the details nafikiri zile hatuwezi kujitaja hapo.

The rights to strike is again the matter of details. Equal rights to strike but under certain circumstances, we have to resource,

lazima umalize zile negotiations. Kuna procedure kwa watu kwamba ukiwa unagombana na tajari, mfuate procedure fulani. Kwa hivyo, labda zile procedure zinahitajia kustahilishwa zaidi, but again it is not a matter to put into negotiation. Ni ufanyi kazi COTU, kupigania kwamba ile procedure ya kufuatwa iwe ya uadilifu zaidi kufuatia Katiba.

Absentee landlords tumepata shtaka hiyo jana pia kwamba mtu amejenga ya ardhi ya mtu mwingine lakini hana hile security of tenure. Hii ni sub-tenancy, you are sub-tenant. Pia hapa sheria lazima iundwe juu ya haki yalio suspended in relation to the landlord. Iwe ni adilifu zaidi pia. May ikiwa siadilifu sasa, au ile jamaa aliyejenga kesho afukushwa na nyumba yake itajenga yapata gharama ya kujenga ya ni mambo ambao bila subsidiary registration can only outlaw, ya kuongeza hiyo zinazo fikiria mambo kama hayo na kustawisha.

Hapa pia kuna tume ingine tatu ambazo inahusika na human rights kama nilivyosema. Tume kama hiyo mtu aweza kuyapelekea mastaka na tume hiyo itaweza kupeleka barua kwa the right department or the right agency groups. Hawo wabunge waambiwe na constituency, mbunge wako alete sheria mbele ya bunge kwamba mahusiano kati ya sub-tenant na mwenye ardhi ambaye ni sasa watu wahulumika nyumba zao zafujwa landlord akitaka ardhi yake anafuja nyumba ya mtu anatupa vitu vyake nje na anafanya atakavyo. That is ile case of – they must having been taken up. Naona shule yetu ni taabu ikiwa kuna nia ya kurekebisha mambo. Mara nyingi mnasema tumelekebisha Katiba, lakini kuna kazi kubwa zaidi, sisi hii ni ile kazi rahisi kabisa. Kazi kubwa zaidi ni kurekebisha akili na nyoyo za watu. Hizo ni lazima zibadilike.

Yule askari ambaye anakulazimisha umpe kitu kabla ya kumpa P3 huyo moyo si mzuri, fikira zake si nzuri. Roho yake si nzuri roho yake ana kudhurumu ile P3 si kuchukuliwa pesa lakini ni lazima tumlekebishe, lazima asomeshwe haki ya mwezake, haki ya raia ni ipi kisa atishwe kwamba akifanya siki nyingine atatiwa ndani. Lakini yule hakimumu ambaye amahukumia hivyo, lazima awe ni honest pia asipate na chake yeye a dismiss ile case au ai-ignore. So we have to change things, we have to change our minds, we have to change our hearts ili kwamba Katiba hii ifaulu. Haiwezi kufaulu it will be just writing on paper, print on paper ikiwa it will not be implemented in the 100%.

This leads to your question. Laws are not follows. Sheria haifuatui, ni kweli. Sheria nyingi ambazo sasa tunalalamika kuwa twafanywa hivi, tufanywe vile sheria iko pale lakini haifuatwi. So what you need is a mechanism, njia au silaha ile huhakikisha kwamba itafuatwa. Na hapo kuna haja ya honesty, uaminifu, uadhilifu na watu ambao wamepewa madaraka fulani kufanya kazi zao bila mapendeleo na kwa nia nzuri.

Abdul Rahman Ali, pia what guarantee kuna dhamana gani kwamba hii sheria itafuatwa? Hatuna dhamana kama nilivyoeleza. Ni watu kukata shauri kwamba tutaifuata.

Court Procedures, Tanzania umesema kwamba ni nzuri kijilinganisha na wenzetu lakini kila nchi itakuwa na sovereignty yake ufalme wake na bila shaka kutakuwa na procedure yetu huenda ikawa ni bora kuliko ile uliona.

Ministry of Lands, ipunguze bei ya ardhi labda tukasaidia kupambana na ufizadi tukifanya hivyo au na mambo mengine ni fikira lakini unajua mambo haya bei ya ardhi na kila kitu is very complicated. You can't law reject like that. Utoe amri acre moja kutoka kesho bei yake itakua hivi. There are all sorts of economic issues na mambo ya uchumi ambayo lazima izingatiwe.

Benson asante sana mambo na masika kwa maoni yako. Graduate employment it is a matter – is a very big problem watu wanamaliza masomo yao hawana kazi – there is an issue of employment, all we are saying kwamba tupate Serikali, systems au mipango ambapo hata ikiwa huna kazi unajipatia ndonge na chakula. And that is a basic needs. Hata huna kazi lakini unapata matibabu ukienda Kenyatta National Hospital, Coast General Hospital, you get the basic medical treatment, mpaka utakapopata kazi.

Shida ya kutokuwa na kazi kutokana, huwa ni kubwa zaidi ikiwa hujui utapa mkate wako lini au wapi. Lakini ikiwa tumepata system, ambayo basic needs zitapatikana kwa kila moja wasi wasi itapungua na tumesema kwamba ingawa hakuna limit zile basic rights tulizozitaja kwa urefu, hapo awali lazima Serikali iazize sasa mpango wa kufanya kuliko kuwapatia wananchi basic needs zao. Ingawa hatukuweka kiwango cha time. Kama nilivyoeleza hapo fixed schedules tumeweka mpango wa time. Jambo hili lifanywe within two years, jambo hili lifanywe within three years.

Basic rights nasema unlimited. Maana siojambo la lahizi kumhakikishia kila mwananchi kwamba atapata matibabu, atapata elimu, atapata makao, atapate maji masafi. Nakumbuka tukisema kwamba water by the year 2000, piped water by the year 2000. Lakini tumepata matatizo ni kweli kikamilifu. Basi, we have to have a target, lazima tuwe na shabaha kufikia pale na tuanze safari ya one thousand, wasema wa-China safari ya one million mine begin with the first step ile first step, second step, ichukuliwe tufikie kule.

Nafikiri Michael sisi tayari education to nursery level. Hapa hatukutaja nursery maana nursery schools nyingi ni private nafikiri. Kwa hivyo hatukuweza kusema kwamba hawa pia watoe elimu ya nursery bure lakini tumepata did you say basic education in primary. Lakini ni fikiria huenda ikazungumzwa na kujadiliwa katika conference.

Each Province to have a university fikira nzuri pesa zikipatikana na official kwamba there is again uadilifu kwamba kukiwa kuna mbili tatu Nairobi itatosheka sasa, tujenge kwengine. Twagenda kislani and that is why Commissions tume zinzohusu human rights and administration of justice tume moja inaitwa hivyo inaweza kusema hapa lazima tupeleke tuwe na kuwapa hali wale pia wapate university. Coast haina university na kadhalika.

Muslim university Coast Province again it is an idea ingawa mujuavyo kwamba kuna mpango wa kujenga university hapa Coast Province ambao itakuwa ni private.

One-third women candidates it is not possible una maoni yako, una haki ya kusema kwamba haiwezekani au ni taabu lakini kuna wale ambao wasemayo inawezakana. Where there is a will there is a way. Ikiwa political parties zataka votes zinategemea wakina mama kesho kina mama tazizia party ambazo haziwasaidea wakina mama kuendelea mbele, votes itakwenda kwingine. May be political parties will be forced to at least consider women candidates.

Na elimu ya MP na elimu na elimu ya councilor ume-suggest should be D+, ndiyo na C again hapo hatukutaja details makusudi.

Twangojea conference labda kuzingatia jambo hili na kufikiria mambo in details. Je ikiwa ni certificate iwe certificate ya C au iwe D.

Refugees in kweli tumepata taabu kutoka kwa wakimbizi na ni kweli vibaya kwamba wakiombizi wanapata IDs za Kenya hapo twarudia mambo haya ya ufisadi, kwamba hawa wanapata IDs kwa ajili ya ufisadi wanamhonga mtu wanajipatia na hapata tegemeo yule administration of our refugees problem. How it is administered na uaminifu uliyoko katika administration ya mambo ya kidini. Again it is a question of reform of the system.

Fikiria za mawaziri ikiwa ni kumi na tano tuhakikishe kwamba wasitoke wote katika province mbili tatu. It is a very good idea tumei-note na bila jambo ambalo litaleta majadiliano mengi sana na majadiliano, ambayo yahistahili kufanywa juu ya distribution of the Ministries between the various provinces.

Nafikiri tumemaliza. Jawabu nawashukuru sana, na samahani nimekwenda mbio katika mambo haya, huenda ikawa nimewacha mambo fulani hapa na pale ambaye ni muhimu lakini ningewasisitiza msome vizuri kuna time ya kupokea reaction zenu, maoni yenu juu ya yaliyomo katika mswada huu wa Katiba tafadhali utataandika hamna haja ya kuweka kwenye posta, district coordinators wetu wawili wako hapa mtawelekea barua kama mlivyofanyia Bwana Daniel ametuachia ile memorandum tutapokea memorandum na tutazingatia mapendekezo yenu baadaye.

Tunawashukuru sana kwa kufika, twafurahi na tumefurahi kwa maswala yenu, na Mungu atusadiye tukamilishe hii kazi kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu na raia wa nchi hii. Tumalize siku ya baraka leo kwa dua tena ili mambo yetu yafanikiwe. Ningemuomba mmoja aje mbele atuombee kufunga kama tulivyooombewa tulivyofungua. Asante.

PRAYER

Basi tusimame na tuombe. Tunakushukuru Mwenyezi Mungu uliye juu Mbinguni, asante kwa sababu tulikupendeza ya kwamba katika nchi yetu ya Kenya, twaweza kuwa na Katiba mpya. Asante kwa sababu umewaongoza viongozi waliochaguliwa katika tume hii. Asante kwa sababu wamekuwa hapa katika hapa sehemu ya Pwani na leo hivi wanamaliza na kurundi yale maoni yote ambao tumetoa wana wapatiye hekima ili wanapoyatekeleza, yaweza kuwa kwa manufaa kwa watu wote wa nchi ya Kenya. Tunaomba haya na kwamini katika jina lako lilo tukufu. Amen.

Meeting ended at 1.15 p.m.

&&